MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Athari ya Miviga Katika Jamii ya Wamakonde Kama Kielelezo cha Utamaduni Zama za Utandawazi: Wilayani Newala Mtwara Tanzania

Olivia Kanwa*

*Idara ya Isimu Na Lugha, Chuo Kikuu cha Bishop Stuart, Uganda.*

## IKISIRI

Makala hii inachunguza jinsi miviga inavyoathiri jamii kwa kuangazia umuhimu wa Miviga katika jamii na matatizo yanayoikumba miviga. Inalenga kubainisha athari za miviga katika jamii ya Kitanzania hasa kabila la wamakonde wa Newala mkoa wa Mtwara katika kipindi cha utandawazi. Maandiko ya wataalamu mbalimbali yamepitiwa ili kubaini kuathiriwa na kuathiri kwa miviga katika jamii za binadamu. Uchunguzi ulifanyika mkoani Mtwara wilaya ya Newala katika kata ya Julia. Vijiji mbalimbali viliyoko katika kata hiyo vimehusika ambapo watafitiwa hamsini (50) kutoka rika zote wametumika katika uchunguzi huu. Data za msingi zilikusanywa kutoka uwanjani kwa kutumia mbinu mbalimbali kama mahojiano, hojaji, ushuhudiaji na ushiriki. Data za upili zilipatikana maktabani kwa kusoma vitabu na tafiti mbalimbali vinavyohusiana na mada hii. Vilevile uchambuzi na uchanganuzi wa data ulifanyika kwa kutumia mbinu ya kiidadi na isiyo kiidadi. Kutokana na uchunguzi huu imethibitishwa kuwa miviga katika jamii ina umuhimu kama vile kuelimisha, kudumisha utamaduni, kuleta jamii pamoja, kuwatahadharisha watu wajiepushe na mikosi na kuburudisha jamii. Pia sherehe za miviga husababisha matatizo mbalimbali katika jamii kama mimba za wasichana wenye umri mdogo, kuongezeka kwa wategemezi, maradhi, ukosefu wa elimu ya afya na kuacha shule. Kutokana na data za nyanjani zinaonesha kuwa suluhisho la matatizo haya ni; elimu kwa jamii, sheria kwa wakiukaji na kuboresha utamaduni kuendane na wakati ni mambo ya msingi katika kupunguza athari za miviga katika jamii ikiwemo jando na unyago. Mwisho makala hii, imetolewa mapendekezo kwa jamii kwa kutoa msisitizo wa kutoa elimu kwa wanajamii. Elimu ni juu ya jinsi ya kuepuka mila zilizopitwa na wakati pamoja na kudumisha tamaduni zenye faida kwa kurekebsha baadhi ya mila ziende na wakati. Mila za kuboresha ni kama vile kuongeza umri wa vijana na mabinti kufanyiwa sherehe za miviga kama vile jando na unyago. Vilevile serikali inafaa kufuatilia wazazi wanaopotosha watoto wao kutoendelea na shule kisa sherehe za miviga ikiwemo maandalizi yake.

## KUHUSU MAKALA

*Maneno Muhimu:*
Athari,
Jamii,
Miviga,
Utamaduni,
Utandawazi.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 27 Oktoba 2025
Tarehe ya Kurekebishwa: 28 Februari 2026
Tarehe ya Kukubalika: 16 Machi 2026
Mtandaoni: 8 Aprili 2026

## 1. Utangulizi

Kazi Miviga ni sherehe mbalimbali katika jamii fulani. Watu hujumuika na sherehe hizi kulingana na tamaduni zao. Watu mbalimbali katika jamii huwa na majukumu tofauti tofauti. Kwa mujibu wa (Wamitila, 2003) Miviga ni sherehe za kitamaduni ambazo huweza kuhusisha matambiko. Miviga hufumbata maigizo ya aina fulani kutegemea sherehe inayohusika. Huandamana na nyimbo, vyakula na mawaidha kutoka kwa wazee. Anataja mifano ya miviga kama sherehe za ndoa, mazishi na tohara. Miviga ina sifa zifuatazo; huandamana na nyimbo zinazohusiana na sherehe hiyo kwa mfano nyimbo za mazishi na ndoa, ngoma mbalimbali huchezwa, pamoja na vyakula vya asili, aghalabu kina mama hupewa kazi za upishi na burudani na wazee hutoa mafunzo na mawaidha kwa vijana. Katika jamii ya wamakonde miviga imeweza kujitokeza kama kitambulisho cha jamii yao kwa kuonesha wanavyojishughulisha katika jando na unyago mkoani Mtwara hususani Newala. Pia imeweza kuleta athari katika jamii hii ya wamakonde kama takwimu inavyoonesha katika miaka ya hivi karibuni. Jambo hili limekuwa likileta athari kwa vizazi tofauti kwa kuzingatia misingi ya kijinsia. (Matinde, 2015).

Takwimu za miaka mitano zinaonesha kuwa wasichana wenye umri mdogo waliweza kupata mimba kutokana na miviga ikiwemo jando na unyago yanayoonyesha kuwa idadi ya wasichana ilifikia 24,236. Inasema mwaka 2020 wasichana wenye umri mdogo waliopata mimba walikuwa 3871, mwaka 2015 walikuwa 4886, mwaka 2016 walikuwa 4616, mwaka 2017

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: kanwaolivia@yahoo.com

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.

Nukuu: Kanwa O. (2026). Athari ya Miviga Katika Jamii ya Wamakonde Kama Kielelezo cha Utamaduni Zama za Utandawazi: Wilayani Newala Mtwara Tanzania. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(1), 15 – 23. https://doi.org/10.61889/1vck0s23.

© 2026 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

walikuwa 4697 na mwaka 2019 ilikuwa 6166. Vilevile takwimu ziaonyesha kuwa walioacha shule kutoka na ujauzito mwaka 2015 walikuwa 421, mwaka 2016 waliacha 297, mwaka 2017 waliacha 230, mwaka 2019 waliacha 197 na hii ilitokana na shughuli za jando na unyago pamoja na mambo mengine ya miviga ambacho ndicho kichocheo kikubwa kwa vijana kujihusisha na masuala ya ngono katika umri mdogo. Wengine walikuja kurudishwa shule ila wengi wao wanakuwa wameishakata tamaa ya kuendelea na masomo kutokana na hali ya uzazi. (https://envaya.org/talia/news) saa 10 jioni 14/7/2022. Hata hivyo (Arege, 2002) anaeleza kuwa kazi za fasihi andishi na simulizi zinapaswa kufanyika kwa kufuata tarataibu mbalimbali. Ndio maana takwimu hizi juu ya athari za jando na unyago zimetolewa kwa kufauata taratibu za mwaka hadi mwaka.

### 1.1. Hali ya miviga katika jamii ya wamakonde.

Shughuli mbalimbali za wamakonde kitamaduni tangu walikotoka huko Msumbiji zimekuwa zikiambatana na ngoma, nyimbo, kula na kunywa kwa siku kadhaa. Kazi za fasihi Simulizi zina tanzu zake ambazo ni ushairi, natiki za Kisasa, semi, methali, ngano, na kadhalika. Fasihi simulizi inatumiwa na jamii kulingana na mila, desturi, elimu na ufundi wa jamii husika. Kila jamii ina mahitaji yake. Elimu ya mafunzo wayapatayo vijana kutoka katika miviga ni sehemu ya fasihi simulizi. Ilianza tangu zamani za mababu zetu. Mafunzo yaliwaandaa vijana na jamii kwa ujumla katika maisha ya kiutuuzima pamoja na kupata maarifa mbalimbali ya kitamaduni.

Gazeti la Mwananchi (10-Oktoba-2010) lilieleza kuwa, Mkuu wa Wilaya Ruangwa Mkoani Lindi na Hawa Mchopa, walipiga marufuku sherehe za miviga ikiwemo jando na unyago kwa mwaka 2010, ili kutoa nafasi ya kila mwananchi kushiriki katika mikutano ya kampeni za uchaguzi mkuu wa Rais na Wabunge. Hiyo ilidhihirisha wazi kuwa viongozi hao wa serikali ambao pia ni wadau wa elimu hawakuona umuhimu wa elimu hiyo katika kuijenga jamii hasa vijana wanaokuwa katika rika la kufuata mikumbo.

Silau (2013), anasema kuwa mafunzo ya miviga kwa kuegemea katika jando na unyago ni kuwa yanasababisha mporomoko wa maadili. Hii inatokea sana baada ya vijana kuhitimu mafunzo hayo. Mporomoko huo wa maadili ya vijana unatokana na mabadiliko ya tabia na mienendo ya vijana siku hadi siku. Hapo zamani vijana walipokuwa wakipata mafunzo hayo ya kitamaduni walikuwa ni msaada kwa jamii. Vijana waliweza kusaidia kazi ndogo ndogo za jamii kama kilimo, kuteka maji mtoni, kukata kuni, kulea watoto wadogo baada ya mama kwenda shambani kwa shughuli za kilimo au kuvuna. Lakini hali hiyo hivi sasa imepotea kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo imeathiri miviga kwa namna fulani. Takwimu za miaka mitano iliyopita za wasichana wenye umri mdogo kupata mimba kutokana na miviga hasa mafunzo ya jando na unyago yanaonyesha kuwa idadi ya wasichana ilifikia 24,236. Mwaka wa 2005 wasichana wenye umri mdogo waliopata mimba walikuwa 3871, mwaka 2006 walikuwa 4886, mwaka 2007 walikuwa 4616, mwaka 2008 walikuwa 4697 na mwaka 2009 ilikuwa 6166. Vilevile takwimu zinaonyesha kuwa walioacha shule kutoka na ujauzito mwaka 2005 walikuwa 421, mwaka 2006 waliacha 297, mwaka 2007 waliacha 230, mwaka 2008 waliacha 197 na hii ilitokana na shughuli za miviga hasa jando na unyago ambacho ndicho kichocheo kikubwa kwa vijana kujihusisha na masuala ya ngono katika umri mdogo (Denscombe, 1998).

Karugendo (2009) akinukuliwa na Rashid (2013) katika tasnifu yake, ameeleza kuwa dini zimekuwa zikipiga vita utamaduni wa jando na unyago. Kwa vile dini hizi ni za kigeni, zilileta utamaduni mpya na kuzika utamaduni wa kiafrika bila kufanya utafiti wa kutosha ili kutoa mabaya na kuacha mazuri. Mtazamo huu unashikiliwa na viongozi wengi wa kidini ambapo wanasisitiza zaidi mafundisho ya dini yanayomjenga mwanajamii katika misingi ya dini Zaidi. Misingi ya dini ikienda sambamba na elimu ya jando na unyago jamii itaimarika. Yote ni mafunzo yanayomjenga kijana katika maadili na mwenendo mwema katika maisha yake. Jamii ya Wahiyao wa Lulindi wanatoa mafunzo yote. Mitazamo ya wadau hawa, imelenga zaidi kuwa miviga na hasa mila ya jando na unyago imeshapitwa na wakati. Ni mila iliyofaa kwa wakati wa zamani siyo sasa. Na kuwa hayo mambo sasa hayawezekani tena. Watoto hawawezi kuwa wanaacha shule kwa sababu ya mila tu zilizopitwa na wakati.

Utafiti wetu, umechunguza mafunzo ya miviga kwa kueleza jinsi nyimbo za jando na unyago na mambo mengine ya miviga yanavyomjenga kijana katika kupambana na maisha ya kiutu uzima. Pia tumechunguza sababu zinazolalamikiwa na wadau mbalimbali juu ya miviga na mafunzo ya jando na unyago yanayosababisha mporomoko wa maadili kwa jamii. Misingi ya fasihi simulizi iliyowekwa na jamii husika hutunzwa lakini pia athari hasi na chanya zimeekwa wazi. Hii inasisitizwa na (Bukenya, 1994) katika kuifanya jamii iijue fasihi simulizi ipasavyo.

### 1.2. Umuhimu wa Miviga

Aghalabu sherehe hizi hufanywa kwa sababu mbalimbali hasa kutunza utamaduni wao katika shughuli mbalimbali za kijamii. Kwa mfano, huweza kufanywa ili kumtoa mtu kutoka katika kundi moja la kijamii hadi jingine Pamoja na umuhimu huo, miviga imekuwa na athari kwa jamii ya wamakonde kutokana na jamii inavyoyapa kipaumbele mambo hayo na kuwafanya kuwa nyuma katika mambo ya kimaendeleo. Watu wengi katika jamii ya wamakonde wamekuwa wakijihusisha na miviga kama kielelezo cha utamaduni bila kujua athari zake. Utafiti huu umekuwa muhimu kuziweka bayana athari za miviga katika jamii za wamakonde wilayani Newala ili ziweze kutambulika na kuwafanya wanaohusika na tamaduni hizo kuwa na mizania katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika jamii zao. Jamii zinapaswa kujua majukumu umuhimu wa fasihi simulizi na kuitumia ipasavyo kwa maendeleo ya jamii (Gibbe, 1998).

### 1.3. Shughuli za kiuchumi za wamakonde

Shughuli kubwa ya kiuchumi kwa Mkoa wa Mtwara ni kilimo, asilimia 85 ya eneo la Mkoa linafaa kwa kilimo.

Shughuli za kiuchumi huwa zinaathiri maandalizi ya miviga kwani wanakuwa wanalazimiaka kufanya kwa muda mfupi ili wakavune. Vilevile shughuli za uchumi ndizo uti wa mgongo wa miviga maana ndiko wanapata pesa za kuwawezesha kufanya sherehe hizi (Rashid, 2013).

Uzoefu unaonesha kuwa sehemu kubwa ya wakazi wa Mtwara katika wilaya zake zote ikiwemo Newala wanajihusisha na kilimo, ambapo asilimia 86 ya wakazi wake hujishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara na chakula ambayo ni korosho, minazi, muhogo, ufuta, mtama, mbaazi, karanga, mpunga, choroko, kunde, nyanya na mahindi. Mkoa umeendelea kufanya jitihada zinazolenga kuhakikisha kwamba wananchi wake wanatumia fursa zilizopo mkoani, kwa maana ya ardhi nzuri na yenye rutuba, hali nzuri ya hewa, miundombinu ya barabara na bandari, nishati ya gesi na umeme na uwekezaji ili kujiletea maendeleo kupitia kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara, ufugaji, ushirika, maliasili na uvuvi. Jamii huwa na shughuli zake katika kuendeleza lugha na utamaduni kwa ujumla (Mlacha, 1995).

### 1.4. Tafiti kuhusu miviga.

Watafiti mbalimbali wamechunguza juu ya sherehe katika jamii za ki-Afrika na hata nje ya jamii za ki-Afrika, hivyo basi, sehemu hii inahusu mapitio mbalimbali yanayohusu miviga, kwa kuangalia utafiti uliotangulia unavyoeleza juu ya suala zima la miviga katika jamii mbalimbali.

Matei (2011), ameeleza kuwa miviga ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalum cha mwaka. Mara nyingi miviga kama vile jando na unyago hufanywa katika kipindi baada ya mavuno. Miviga ya mazishi kwa mfano hufanywa kabla ya wakati fulani wa siku kutegemea imani ya jamii. Aidha miviga ya kuwapa watoto majina huadhimishwa muda fulani baada ya mtoto kuzaliwa. Miviga huandamana na matendo au kanuni fulani (viviga), hufuata utaratibu maalum na huwa na sababu maalumu. Utafiti huu umetoa mwanga kuhusu vipengele vya miviga na sababu zake. Vile vile utafiti huu umekuwa ni chachu ya kufanya utafiti juu ya athari za miviga maana jambo ambalo limeachwa kando. Wathome (2009), katika utafiti wake wa shahada ya uzamili kuhusu nyimbi za tohara za jamii ya wakamba nchini Kenya, anaeleza kuwa nyimbo za tohara katika jamii hizo zinaimbwa ila kisasa zaidi na pia zimepoteza mwelekeo kulingana na maendeleo ya sayansi ya teknolojia kwani zinaonekana kupitwa na wakati. Vijana bado wanafanyiwa tohara ila wanapelekwa hospitali siyo kutahiriwa na ngariba tena kama ilivyokuwa awali. Utafiti huu umekuwa chachu kubwa ya kufanya utafiti huu wialayani Newala juu ya athari za miviga katika jamii ya wamakonde. Kama jamii ya wakamba imebadilika katika mambo ya kitamaduni, je ni kwa vile wanajua athari za miviga au la? Hili limewekwa bayana katika utafiti huu juu ya mada lengwa. Matei (2011), anafafanua kuwa iviga kama aina ya sherehe fulani ambayo huambatana na matendo fulani hutofautiana toka jamii moja hadi nyingine kutegemea na kanuni na desturi za jamii hiyo husika. Mfano katika kabila la kimasai huwa na sherehe (miviga) katika suala zima la jando na tohara (unyago). Miviga huongozwa na watu mahsusi ambao huendeleza shughuli za miviga katika sherehe mbalimbali mfano za kidini, kafara, jando na unyago, sherehe za kilimo na mazishi (misiba) lazima panakuwa na mtu au watu maalum ambao huongoza au huwa wasemaji wakuu ambao huchukuliwa kuwa viongozi wa sherehe hizo. Watu hao wanaoongoza shughuli za sherehe hizo huwa wana ujuzi na maarifa juu ya jambo hilo. Mfano katika sherehe za tohara ambazo huongozwa na ngariba ambaye ana ujuzi juu ya jambo hilo. Utafiti huu umekuwa wa muhimu kwetu kwani umeeleza miviga inayofanywa katika jamii za wamasai ingawa athari zake hazijawekwa bayana. Utafiti huu umekuwa ni wa muhimu katika kuchunguza athari za miviga katika jamii ya wamakonde wilayani Newala.

## 2. Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanyika mkoani Mtwara wilaya ya Newala katika kata ya Julia. Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka eneo tajwa japo zingeweza kukusanywa kutoka eneo lolote mkoa wa Mtwara, katika wilaya yoyote maana shughuli zifanywazo na wamakonde wa mkoa huu wa Mtwara zinafanana na tamaduni zinazoshabihiana kwa ukaribu. Lengo la kuteua eneo hilo ni sababu za kiuchumi kulingana na uzoefu na uenyeji wa mtafiti maana wilaya ya Newala ndiko aliweza kufika na kukusanya data kwa urahisi kuliko sehemu nyinginezo. Eneo hilo limechaguliwa kimaksudi kuwakilisha mkoa wa Mtwara na wilaya nyingine wanamoishi wamakonde wanaoendelea kufanya sherehe za miviga kama kiwakilishi cha utamaduni wao. Umuhimu wa kuteua eneo hili ni kwa ajili ya kuakisi uhalisia wa mada katika eneo husika (Cohen, 2001; Denscombe, 1998).

Utafiti ulitumia data za aina mbili; za msingi na za upili. Za msingi zilipatikana kwa kutumia mbinu za mahojiano na ushuhudiaji ambapo mahojiano yalihusisha wazee wanaofundisha mambo mbali mbali ya miviga kama kielelezo cha kitamaduni zikiwemo jando na unyago, ngoma, nyimbo na mavazi. Vijana wanaosherehekea na kuwajibika kwa umoja wao, wake kwa waume, viongozi wa vikundi vya kijamii katika vijiji (koo) zao nao walihojiwa. Wazee ndio wanaojua mila na desturi yakiwemo mafundisho ya rika kwa rika pamoja na nyimbo za aina mbalimbali zikiwemo zinazotumiwa katika sherehe za miviga. (Kothari, 1993; 2008)

Wazee ndio huwafundisha vijana na watu wa rika mbalimbali namna ya kufanya sherehe za miviga ambazo huwa ni kama mashindano ya koo na koo katika kuonesha kufana kwake kwa kuwa na wahudhuriaji wengi, vyakula na burudani kedekede na namna wanavyotumbuiza wakati wa kuonesha au kuwatoa wari ndani au waliofanyiwa tohara au wakati mwingine wafiwa Hapo ndipo huwa patashika nguo kuchanika au asiyekuwa na mwana aeleke jiwe. Rika zote huhusishwa katika nyimbo za sherehe za miviga (Waziri, 2016). Mbinu ya ushuhudiaji imetumika katika kukusanya nyimbo zinazoimbwa wakati wa shrehe za miviga kuanzia siku ya kwanza mpaka ya tatu wanapotolewa nje wari, waliotahiriwa au wafiwa.

Data za upili zilikusanya kwa kupitia nyaraka za maktabani kuhusu jamii za wamakonde na shughuli zao za kijamii na kiuchumi. Vilevile zimepitiwa nyaraka kuhusu tafiti mbalimbali za fasihi simulizi kuhusu miviga na nyimbo ambazo zinahusu tamaduni mbalimbali za Kiafrika hususani wamakonde katika mikoa ya Kusini mwa Tanzania. nyaraka zote hizi zimesaidia kujenga uelewa juu ya mada ya utafiti ambayo ni athari za miviga katika jamii za wamakonde kama kielezo cha utanaduni katika zama hizi za utandawazi katika jamii ya wamakonde. Ni muhimu kutafiti fasihi simulizi na kutambua mambo mbalimbali yanayohusu nyimbo mbalimbali na athari zake kwa jamii (Mutwiri, 2005; Yego, 2011).

Hata hivyo katika upitiaji nyaraka imebainika kuwa miviga imetafitiwa kwa uchache katika jamii za wayao (Rashid, 2013), Ubabedume katika majigambo ya miviga ya shilembe, (Kibigo, 2020), Nyiso za wabukusu, (Simiyu, 2007), Nafasi ya muktadha katika utendaji wa miviga ya Olubeko, (Waswa na wenzake, 2022). Ingawa miviga ya jamii mbalimbali za kiafrika imetafitiwa kwa uchache, ila hazijatafitiwa kwa upana wake. Nyaraka hizi zimekuwa msaada katika kupata maarifa ya miviga kwa ujumla na kutoa mwanga wa kukiendea kile ambacho ni lengo la utafiti huu.

Maktaba zilizotumika ni za Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam hasa sehemu ya East Afrikana ambako ni sehemu ya tafiti mbalimbali, maktaba kuu ya taifa, maktaba ya Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Mwanza pamoja na maktaba ya Chuo Kikuu cha Bishop Stuart Mbarara Uganda. Maktaba hizi zimejaa nyaraka mbalimbali zilizotoa data zilizokuwa zinahitajika katika kukamilisha utafiti huu.

Jed. 1: Umuhimu wa sherehe za miviga katika jamii ya wamakonde

| Umuhimu | Idadi Ya Wahfojiwa | Asilimia Za Wahojiwa |
|---|---|---|
| Huleta jamii pamoja na kuunganisha jamii | 15 | 30 |
| Huelimisha na kufundisha jamii | 5 | 10 |
| Hudumisha tamaduni katika jamii | 20 | 40 |
| Huburudisha | 5 | 10 |
| Kuwatahadharisha watu wajiepushe na mikosi | 5 | 10 |
| JUMLA | 50 | 100 |

***Chanzo: data za nyanjani (2022)***

## 3. Umuhimu wa sherehe za miviga katika jamii ya wamakonde.

Utafiti ulifanyika katika wilaya ya Newala mkoa wa Mtwara ambapo wahojiwa mbalimbali wenye hadhi tofauti walihusika kutoa taarifa au data ambazo zinahusiana na umuhimu wa sherehe za miviga ambazo zinafanyika katika maeneo mengi ya jamii yetu. Jed. 1 linatoa muhtasari wa matokeo kuhusu umuhimu wa sherehe za miviga

### 3.1. Huleta jamii pamoja na kuunganisha watu katika jamii.

Kutokana na utafiti uliofanyika imethibitika kuwa shughuli za jando na unyago watu hukutanika pamoja ili kujenga masuala mbalimbali katika jamii ikiwemo kuunganisha jamii na watu mbalimbali ambapo asilimia 30 ya wahojiwa wamethibitisha ukweli kwamba jando na unyago huunganisha watu katiuka jamii. Kwa hiyo kupitia shughuli mbalimbali za kijadi kama sherehe za mazishi na ngoma, ndoa, jando, unyago na mavuno kupitia sherehe hizi watu hudumisha udugu na kujenga ujamaa. Tak. hapo chini iliyoambatanishwa inaonesha watu wa rika mbalimbali wakishiriki sherehe kwa kucheza pamoja ngoma za kitamaduni wakimfurahia mwari kutolewa nje. Katika mazingira ya kijamii rika zote huchanganyika katika kuadhimisha jambo. Hii ndiyo fasihi simulizi ambayo jamii inapaswa kuijua na kuiendeleza siku hadi siku kwa kuzingatia maendeleo ya jamii (Nandwa & Bukenya, 1983).

Katika jamii ya wamakonde, hii ni sherehe kubwa ambapo watu hualikwa kushiriki kucheza kula na kunywa. Pamoja na kuwa wanaohudhuria ni watu wa rika zote, Tak.ni tunaona kuwa wanaocheza ni watu wa umri tofauti na jinsia tofauti wote hucheza pamoja kama njia ya kuwaweka pamoja na kujenga mshikamano wa kijamii. Kulingana na nadharia ya ethnografia ya mawasiliano mhimili usemao mada au jambo linalozungumzwa ni muhimu kuzingatiwa. Katika hoja hii ni kuwa jamii inakutana pamoja kwa ajili ya kuimba na kushereheka pamoja na kuwashangilia watoto waliomaliza mafunzo ya kutoka rika moja kwenda rika linguine. Vile vile mhimili unaosema kuwa lugha na yote yanayotendeka yanapaswa kuendana na utamaduni. Kama inavyoonekana katika Tak. 1, wanaocheza wanavaa mavazi ya kitamaduni na nyimbo za mila na desturi huimbwa. Mfano wanaume kujifunga vitenge viunoni wakati wa kucheza. Haya mavazi huonesha mila na desturi katika nyimbo mbalimbali (Ngure, 1998).




Tak. 1: Mavazi yanayosawiri mila na desturi.

### 3.2. Huelimisha na kufundisha jamii.

Kupitia miviga watu hutoa mafunzo mbalimbali ambayo hufikishwa kutokana na sherehe husika, mfano katika mazishi wosia mbalimbali hutolewa, pia katika ndoa ujumbe mbalimbali hutolewa kwa wanandoa kuhusiana na maisha ya familia, vilevile katika sherehe za jando na unyago vijana huaswa mambo yahusuyo utu uzima. Haya ni mambo ya msingi ya mila na desturi katika jamii yanayozingatiwa na kila rika (Mohamed, 2016).

Katika utafiti wetu silimia 10% ya wahojiwa wamethibisha kuwa katika sherehe za miviga haswa jando na unyago vijana wengi hupewa mafuzo na maadili mbalimbali ili kukabiliana na maisha katika jamii inayowazunguka na mafunzo hayo huwa msaada mkubwa kwa vijana na wahudhuriaji wote. Nadharia ya ethnografia ya mawasiliano katika mhimili unaoelezea wahusika. Tak. 2 inaonesha wahusika watoto wa rika moja ambao wametoka kupata elimu rika na kuwafanya waweze kuishi katika jamii kwa kufuata waliyofundishwa. Mafunzo haya watayaishi na baadae kuwafunza watoto wao watakapokuwa wakubwa (Sanken, 1976).



Tak. 2: Vijana wa kike waliopakwa majivu kuashiria hatua mpya ya makuzi.

### 3.3. Hudumisha tamaduni katika jamii.

Katika Tak. 3 tunaona watoto wanaotolewa ndani wakiwa wamepakwa rangi nyeupe usoni na kuvalishwa mavazi ya kitamaduni. Kama inavyoeleza nadharia ya ethnografia ya mawasiliano katika mhimili unaosisitiza utamaduni. Rangi nyeupe kitamaduni ni utambulisho kuwa watoto hao kuwa ni weupe na mioyo yao ni myeupe bado ni wasikivu, watii, wachapakazi na hawajaanza kujishirikisha katika mambo ya kuwachafua kitabia kama vile kufanya ngono, kutoroka nyumbani, kukwepa kazi, kutukana watu wa rika tofauti na tofauti. Wameshikishwa fimbo mkononi kama silaha ya kujilinda na kuyapinga mabaya yote ya kuwafanya waende kinyume na mafunzo yote waliyopata kutoka kwa wakubwa wao, wazazi na wataalamu wa miviga wanaotoa mafunzo hayo. Mafundisho haya ni mazuri kulingana na mila na desturi japo wanapoyatumia vibaya wanaangamia na kushindwa kusoma. (Mamuya, 1972).



Tak. 3: Ushirikiano miongoni mwa vijana waliofanyiwa jando na unyago

Tak. 3 pia inaonesha umoja na mshikamano miongoni mwa watoto hawa ikiwemo kula pamoja na kushiriki vyakula vya asili bila kubaguana, kuwa na uchoyo na kupendana miongoni mwao. Wameaminishwa kuwa mabaya hayatawapata dhidi ya walimwengu kwa kuwapaka madawa mbalimbali katika miili yao na kuwafunga viunoni na wengine mikononi.

Utafiti unaonyesha kuwa mila na desturi katika jamii hudumishwa kupitia shughuli mbalimbali zikiwemo ngoma za asili, jando na unyago, ndoa, matambiko na shughuli za kutawazwa kwa viongozi wa kijadi, wahojiwa ambao ni asilimia 40% kutoka sehemu mbalimbali za maeneo ya Newala katika kata tajwa wamethibisha kuwa sherehe hizi za jando na unyago zinadumisha tamaduni za wamakonde ambazo hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Kwa mfano sherehe za jando na unyago katika maeneo ya Mtwara haswa Newala hufanywa kipindi cha mwenzi wa sita na wa saba ambapo wakati huo huwa ni kipindi cha mavuno ya mazao ya muda mfupi na watoto huwa katika likizo na kipindi cha mwezi 10 na 11 wanapokuwa na pesa za mavuno ya korosho ndipo sherehe nyingi hufanyika. Kwa hiyo basi, kupitia miviga mila na desturi za jamii husika hudumishwa kwa kuendeleza jamii kama vile katika sherehe mbalimbali za kijamii huwepo vyakula mbalimbali vya kiasili kama katika jamii ya wanyakyusa “kisyesye” ni mkate uliotengenezwa na mahindi mabichi yaliyotwangwa. Pia kwa waha kuna kinywaji aina ya pombe iitwayo “kayoga” ni pombe ya asili itengenezwayo kwa ndizi na ulezi ni kinywaji kipendwacho katika sherehe mbalimbali (Wamitila, 2003).

### 3.4. Kuburudisha jamii.

Wanajamii wakiburudika wakati wa sherehe za miviga baada ya kula na kunywa kwa pamoja. Tak. inaonesha jinsi washiriki wa rika zote wanavyocheza ngoma za kitamaduni kwa furaha kuu

Miviga ni sherehe ambazo hufanyika kwa ajili ya madhumuni mbalimbali ambazo hufanywa katika jamii kama vile ndoa, matambiko, jando na unyago ambapo

mkusanyiko huo unahusisha ngoma mbalimbali za kijadi zinachezwa na hufanya watu mbalimbali kukusanyika pamoja na kuburudika kutokana na ngoma hizo. Katika utafiti huu asilimia 10 ya wahojiwa wamethibitisha kuwa sherehe hizo za miviga zinaburudisha watu mbalimbli ambapo ngoma mbalimbali hupigwa na kuchezwa na watu mbalimbali kama vile singenge, mnanda, mdundiko na beni ambapo wachezaji wengi huvaa nguo za asili na vinyago ambapo watu hucheka na kufurahi kutokana na ngoma hizo. Kwa hiyo, miviga huburudisha pindi inapohusisha nyimbo na michezo ya kuigiza katika sherehe mbalimbali za kijamii, mfano katika kabila la wasukuma kipindi cha mavuno ngoma mbalimbali aina ya "mbina" huchezwa ngoma hizi dhumuni lake ni kuburudisha na kuwaleta wana jamii pamoja kama wafanyavyo wamakonde. Jamii inapaswa kuijua fasihi simulizi ipasavyo ili kuzingatia mazuri yake na kuyaendeleza kwa ajili ya vizazi vijavyo (Juma, 2015).



Tak. 4: Burudani za ngoma za kijadi miongoni mwa wanajiamii.

Nadharia ya ethnografia ya mawasiliano katika mhimili unaoeleza ujumbe unaotolewa kulingana na lengo la kusanyiko. Tak. 4 inasawiri wanajamii wakiburudika baada ya kuwapa mafunzo ya rika vijana wao. Jamii inaungana kwa umoja kushiriki tukio hilo la kijamii ambalo halina ubaguzi wa aina yeyote kirika, kijinsia na kiuchumi.

Vilevile katika kabila la waha kuna ngoma ya "ubhusambele" ambayo huchezwa katika sherehe mbalimbali za kijamii pia wanyakyusa wana ngoma iitwayo "magosi" na "samba" zote hizi huchezwa katika kipindi cha mavuno ambazo huwaweka pamoja wana jamii na kuwaburidisha.

### 3.5. Kuwatahadharisha watu wajiepushe na mikosi.

Kutokana na utafiti inadhihirika kuwa shughuli za jando na unyago hufanyika ili kutoa tahadhari ya masuala fulani wanayoyaamini katika jamii hiyo. Kwa mfano katika jamii ya kimakonde binti asipofanyiwa unyago hufahamika kuwa binti huyo bado hajakomaa na pia ataleta mkosi katika jamii, asilimia 10 ya wahojiwa walikubali hoja hiyo. Pia kupitia miviga watu hutambulishwa ili wasikumbane na maafa. Mfano mtu akiwa jikoni moshi ukaelekea upande wake humaanisha kuwa mtu huyo anajisaidia njiani hii ni kwa watu wa jamii za "Wanyaturu" na "Waha", pia kwa waswahili wanaamini ukienda chooni usiku bila taa utapigwa na kitu kisichojulikana. Mambo haya ni muhimu kufanyiwa utafiti siku hadi siku ili kuitahadharisha jamii kwa kuwapa takwimu za athari ili wawaeze kuelewa (Kothari,2008).

Kwa kurejelea nadharia ya ethnografia ya mawasiliano inavyosisitiza muktadha na utamaduni, watoto wanapopewa mafunzo ya rika pia kuna masuala ya imani ya kiasili au kikale yanayotoa msukumo katika kufanya miviga. Huamini kuwa watoto wasipofanyiwa miviga huko mbeleni katika maisha watakumbana na balaa na mikosi. Hivyo wazazi husukumwa kufanya miviga kwa ajili ya mambo kama hayo.

### 3.6. Matatizo ya jando na unyago katika jamii

Matatizo haya katika jamii ya wamakonde hayaepukiki kwa kiasi kikubwa kutokana na shughuli za miviga hasa jando na unyago inavyojidhihirisha. Jed. 2 ni muhtasari wa matokeo kuhusu matatizo ya jando na unyago.

Jed. 2 : Matatizo ya jando na unyago katika jamii.

| Matatizo | Wahojiwa | Asilimia |
|---|---|---|
| Mimba za utotoni | 20 | 40 |
| Kuongezeka kwa wategemezi | 5 | 10 |
| Maradhi | 10 | 20 |
| Ukosefu wa elimu ya afya | 5 | 10 |
| Kuacha shule | 10 | 20 |
| Jumula | 50 | 100 |

***Chanzo:data za nyanjani (2022)***

#### *3.6.1. Mimba za utotoni*

Utafiti unaonesha kuwa mimba za utotoni ni tatizo kubwa nchini Tanzania hasa mikoa inayofanya sherehe za mila(miviga). Kwa mujibu wa wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi wasichana 8000 kila mwaka huacha shule kutokana na ujauzito. Kati yao wanafunzi 3000 ni wanafunzi washule za msingi (Rashid,2013).

Kutokana na utafiti, tatizo la mimba za utotoni mkoani Mtwara linasababishwa na shughuli za kijadi za miviga kama jando na unyago kwasababu katika shughuli hizo watoto hufundishwa masuala ya ndoa na hivyo hupelekea kufanya matendo ya ndoa baada ya kutoka huko, 40% ya wahojiwa wamekubali hoja hii. Kwa mujibu wa Silau (2013) na Rashid (2013), mimba za utotoni wilaya ya Newala Mkoa wa Mtwara bado ni tatizo ambalo husababishwa na sherehe za miviga ikiwemo jando na unyago. Katika nadharia ya ethnografia ya mawasilaiano tunaona kuwa mada inakuwa ni kutoa mafunzo ya kutoka rika moja hadi lingine lakini kunakuwa na lengo fiche ambalo linakuwa ni kuwapa elimu ili kuwaepusha na mambo mbalimbali mabaya kwao kulinagana na umri ikiwemo mimba za utotoni.

#### *3.6.2. Kuongezeka kwa wategemezi*

Utafiti unaonyesha kuwa vijana wengi wanapotoka kwenye jando na unyago hawafundishwi mbinu za kujikimu na maisha yao ya baadaye hivyo hukosa uwezo wa kujikimu kimaisha na kuwa wategemezi kwa wazazi wao na kuongeza mzigo mwingine kwa familia. Hii huwafanya wazazi kuwa waangalifu sana la sivyo kutakuwa na watoto wengi wasiojulikana baba zao na

kuwa wategemezi kwa wazazi wa mtoto wa kike (Mlambia, 2017). Asilimia 10 ya wahojiwa wamethibitisha kuwa tatizo hili la utegemezi linachangiwa na mafunzo ya jando na unyago ambayo yanajikita sana katika kufundisha masuala ya ndoa.

### 3.6.3. Maradhi

Vijana wengi hupata maradhi kutokana na mafunzo ambayo wanapewa katika shughuli za miviga ikiwemo jando na unyago ambapo wasichana wengi hupata ugonjwa wa fistula kutokana na kujifungua katika umri mdogo. Mafunzo hayo hayatoi tahadhari kwa vijana na suluhu ya kukabiliana na maradhi hayo bali huchochea mihemko katika suala zima la ngono katika umri mdogo. Asilimia ishirini (20%) ya wahojiwa wamethibitisha kuwa jando na unyago ni kichocheo cha maradhi ya fistula kwa vijana wadogo katika jamii. Daktari Ndungile, ambaye alikuwa daktari wa hospitali wa wilaya alipohojiwa mwaka 2022 anathibitisha kuwa wajawazito wengi ambao wanakuja kujifungua chini ya umri usiositahili ambao hupelekea kupata ugonjwa wa fistula. Nadhara ya ethnografia ya mawasilaiano mhimili wa sababu za mawasiliano lengwa. Kila jambo hufanywa kwa sababu fulani. Watoto wanapopewa elimu rika pia wanafunzwa kuhusu maradhi yatakayowakumba endapo hawatazingatia waliyofundishwa ikiwemo kupata maradhi katika umri mdogo. Haya yamesisitizwa na Senyamaza ambaye alikuwa afsa ustawi wa jamii katika wilaya ya Newala mwaka 2015 alipohojiwa alifafanua na kurejelea maendeleo ya jamii na mabadiliko ya mambo mbalimbali ya kushangaza katika jamii za wilaya ya Newala.

### 3.6.4. Ukosefu wa elimu ya afya

Wazee wengi wa jadi wanaotoa mafunzo hayo huwa hawana elimu ya kutosha kuhusiana na afya hivyo basi mafunzo hayo huambatana na elimu ndogo kuhusu afya. Wanapaswa kuepwa elimu juu ya jinsi ya kujikinga na maradhi na kusababisha vijana wengi kuingia katika mambo makubwa bila ya kujua athari zake kiafya na jinshi ya kuyatatua. Wahojiwa 5 ambao ni asilimia 10 wanathibitisha kuwa ukosefu wa elimu ya afya katika mafunzo ya jando na unyago huleta athari kubwa ya kiafya kwa vijana wa jinsia zote katika jamii ya wamakonde wilayani Newala. Kwa mujibu wa mkurugezi mtengaji wa Newala Bi. Christina Kambuga mwaka 2004; mimba za utotoni zinachangia elimu duni na umasikini wilayani Newala. Haya yamefafanuliwa zaidi na Rashid (2013), wakati akifafanua masuala mbalimbali ya kijamii katika jamii ya Wahiyao wilayani Masasi. Nadharia ya ethnografia ya mawasilano mhimili wa misingi ya utamaduni unatueleza kuhusu kutoa elimu ya kitamaduni na kwenda nje ya hapo. Suala la kwenda nje ya utamaduni hutegemea masuala ibuka. Watoto wa kizazi hiki wanafaa kupewa elimu juu ya afya zao na namna ya kujitunza wasikumbwe na magonjwa ya zinaa na mengine mengi.

### 3.6.5. Kuacha shule

Shughuli za jando na unyago haitoi kipaumbele katika suala la elimu bali hutoa kipaumbele katika kufundishwa suala la ndoa hivyo inajengeka akilini mwao kuwa wana uwezo wa kupata watoto. Utamaduni ambao kipaumbele chake si elimu huleta shida na kufanya vijana wengi kuacha shule na kujishughulisha na masuala ya mahusiano.

Utafiti huu unaonyesha kuwa wazazi nao wanachangia watoto wao kukatiza masomo na hatimaye kupata ujauzito. Asilimia 20 ya wahojiwa wanadai kwamba wazazi huwatorosha watoto wao pindi wanapofaulu na kuwaoza. Mwaka 2020 watoto 47 walifaulu lakini hawakwenda shule, wanatoroka, wanaolewa na kupata mimba. Kwa mujibu wa Mussa (2023), anaeleza kuwa mimba za utotoni wilaya nyingi za mikoa ya Pwani mwa Bahari ya Hindi ikiwemo wilaya ya Newala Mkoa wa Mtwara bado ni tatizo ambalo husababisha na sherehe za jando na unyago. Hivyo husababisha watoto wengi kuacha shule.

Nadharia ya ethnografia ya mawasilano inaeleza kuhusu kutumia lugha katika mawasiliano. Katika elimu wanayopewa watoto katika rika lao moja wapo ni kusisitizwa umuhimu wa shule kwani wengi wao wakifanyiwa miviga hupuuza elimu na kujiona wamekuwa wakubwa na mashujaa wa kijamii.

## 3.7. Kubainisha njia za kuweza kuondoa athari hasi za miviga.

Utafiti unapendekeza kuwa matatizo yanayosababishwa na miviga katika jamii yanaweza kutatuliwa kwa njia anuai. Jed. 3 ni muhtasari wa mapendekezo haya.

Jed. 3 : Njia za kuweza kuondoa athari hasi za miviga katika jamii.

| Njia Za Kuweza Kuondoa Athari Za Miviga | Wahojiwa | Asilimia |
|---|---|---|
| Elimu kwa jamii | 20 | 40 |
| Sheria kwa *wakiukaji* | 10 | 20 |
| Kuboresha tamaduni ziendane na wakati | 20 | 40 |
| JUMLA | 50 | 100 |

***Chanzo:data za nyanjani (2022)***

### 3.7.1. Elimu kwa jamii

Kutokana na utafiti inadhihirika kuwa elimu imekuwa ikitolewa kwa bidii na wanawake kutoka umoja wa wanawake na wa mkoa wa Mtwara na maofisa maendeleo ya jamii. viongozi hawa kwa kushirikiana wamekuwa wakizingumza na wanafunzi wa kike shuleni. Hali hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kubadili mielekeo ya wanafunzi kuhusu suala la elimu. Hivi sasa wasichana wengi wamekuwa wakimaliza elimu ya darasa la saba ikilinganishwa na awali (Mussa, 2023). Asilimia 40 ya wahojiwa wanakubali kuwa elimu inayotolewa katika jamii inayohusu masuala ya jando na unyago imetia hamasa ya vijana kendelea na masomo.

### 3.7.2. Sheria kwa wakiukaji

Utafiti unaonyesha kuwa ili kuboresha masuala ya kiafya na elimu katika jamii lazima kuwepo na sheria na kanuni zinazo pinga masuala halisia ya athari zinazotokana na jando na unyago. Pia serikali itoe onyo n ahata adhabu kwa wale ambao wanawaambia watoto wao wasifaulu ili waolewe, kitu ambacho kitachangia kuleta athari kubwa au upungufu mkubwa wa wasomi katika nyakati zijazo. Hii inashadidiwa na Saleh (2015), anapoeleza masuala ya ufasihi simulizi katika fasihi andishi na kuonesha kuwa suala la ufuataji sharia katika masuala ya fasihi simulizi ni la muhimu. Asilimia 20 ya

wahojiwa wanasisitiza kuawa lazima serikali itoe msimamo na sheria ambazo zitasaidia kupunguzsa suala la utoro shuleni.

### *3.7.3. Kuboresha tamaduni ziendane na wakati*

Tak. 5 ni kijana aliyefanyiwa sherehe za miviga kutokana na mafunzo aliyoyapata ni kuwa anapokuwa anakula ni sharti kukaa chini. Kulingana na mabadiliko ya wakati sasa si kukaa chini bali ni kwenye kiti cha kimila kama Tak. inavyoonesha. Sylvester (2015), anasisitiza kuwa nyimbo mbalimbali za kijamii huwafundisha vijana wa kike na wa kiume kuzijua taratibu za kijamii na kuziishi.



Tak. 5: Kuketi wakati wa mlo ni kutii utamaduni.

Katika nadharia ya ethnografia ya kimawsiliano tunaona kuwa utamaduni ni kitu cha msingi sana katika maendeleo ya jamii. Kutokana na tamaduni nyingi za kitanzania kutokwenda na wakati na kutovipa kipaumbele vitu vyenye msingi ambavyo vitasaidia maendeleo katika jamii na tamaduni za sasa hazina budi kubadili mfumo huo na kutilia mkazo masuala ya msingi kama elimu na vijana. Badala ya vijana kufundishwa suala la ndoa tu katika miviga hasa jando na unyago, wafundishwe pia elimu kuhusu afya ya uzazi, mbinu za kujitegemea na kutilia mkazo kuhusu elimu ya darasani. Asilimia 40 ya wahojiwa wametilia mkazo suala la elimu na kusema uboreshwaji wa tamaduni hizo kutaondoa kabisa athari zinazotokana na mila hizo. Tamaduni ni jambo la msingi katika ustawi wa jamii na kuwa kielelezo cha maendeleo Wamitila (2008).

## 4. Hitimisho

Kila jamii ina utamaduni wake ambao haupaswi kuachwa kutokana na manufaa yake katika jamii hiyo. Hata hivyo jamii inapaswa kubadilika kulingana na wakati ili kuifanya jamii hiyo isiwe nyuma kimaendeleo katika nyanja mbalimbali kutokana na kujikita katika ukale zaidi. Kwa mfano kama jamii katika wilaya ya Newala na sehemu nyinginezo za mkoa wa Mtwara huwa na sherehe mbalimbali za miviga ikiwemo jando na unyago kila mwishoni mwa mwaka. Shughuli huhusisha kuwapeleka vijana wa kike na wa kiume porini kwa muda wa siku zisizopungua 14 ili wapate mafundisho. Wakishatoka hufanyiwa sherehe kubwa kuhitimisha mafunzo hayo na jamii ishuhudie kuwa vijana wamefuzu mafunzo hayo. Kutokana na kasi ya watu kuhamia mkoa wa Mtwara sababu ya uvumbuzi wa gesi na mafuta pamoja na kiwanda cha saruji cha Dangote hivyo mwingiliano wa watu wenye tamaduni tofauti tofauti. Hii itawabadilisha watu wa Mtwara na kuwafanya waweze kwenda na wakati kuhusiana na masuala ya miviga tofauti ilivyokuwa awali. Hali hii hubadilika kutokana na mwingiliano wa watu wenye tamaduni tofauti.

Kama ilivyooneshwa katika tafiti za Waswa na wenzake (2022), Kibigo (2020), na Simiyu (2007). Matei (2011), Rashid (2013), Mohamed (2016), Wathome (2009), na Waziri (2016) na wengineo wengi wameonesha kuwa tamaduni za jamii mbalimbali walizozifanyia utafiti zinabadilika lulingana na wakati. Wengi wao wanaeleza kuwa katika kushughulikia tafiti zao wamegundua kuwa kuna mabadiliko tofauti tofauti katika jamii. Kila jambo ni muhimu lifanywe kwa kufuata misingi na kanuni zake hata ikiwa ni za kitanaduni au za kitaaluma katika kuzitafiti na kuzifanyia kazi (Enon,1998).

Kuna ambao bado wanashikilia ukale na kutopokea mabadiliko na kuifanya jamii kuendelea kupishana na utanadawazi na pia zipo jamii zilizobadilika na kuacha kabisa tamaduni zao nje na kushika umagharibi. Mabadiliko haya yanatokana na jamii kuona kuwa tamaduni zao zimepitwa na wakati na hivyo kuziacha kabisa na wengine kuzifanya katika hali ya usasa isiyotambulisha utamaduni wao kama jamii za kiafrika. Mabadiliko haya hupelekewa ba mfumo wa elimu ya sasa, dini za Kimagharibi, maendeleo ya sayansi na teknolojia, pamoja na tamanduni za kigeni. Wako ambao wamezishika tamaduni zao na kuziendeleza sambamba na utandawazi (Mbogo, 2008).

Utafiti huu umebaini kuwa jamii inatakiwa kuwa na mizania katika mambo yote haya ili yaweze kwenda pamoja yaani utamaduni wa kiafrika pamoja na utandawazi (sayansi na teknolojia).

## Marejeleo


Arege, T. (2002). Mwongozo wa Kilio cha Haki. Nairobi: SAT Publishers.

Bukenya, A. (1994). Understanding oral literature. Nairobi: Nairobi University Press.

Cohen, L. L. M., & Keitle, M. (2001). Research methodology education. London: Routledge Farmer.

Denscombe, M. (1998). The good research for small social research projects. Buckingham: Open University Press.

Enon, J. C. (1998). Educational research statistics and measurements. Kampala: Makerere University.

Gibbe, B. (1998). Social roles and participation in society. Bruxelles: Pierre Mardaga.

Juma, N.F. (2015) Nyimbo za harusi na maadili ya ndoa za

Wapemba, (Tasnifu za Uzamili, Chuo KIkuu cha Nairobi), {Haijachapishwa}

Karugendo,P.(2009). Bikira Yangu. Dar Es Salaam, Shule & Company

Kibigo, M. L. (2020). Ubabedume katika majigambo ya miviga ya Shilembe na Mchezasili wa Mayo miongoni mwa Waisukha nchini Kenya kwa mtazamo wa Kisemantiki (Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro). [Haijachapishwa].

Kothari, C. R. (1993). Research methodology: Methods and techniques. New Delhi, India: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R. (2008). (2nd ed.). Research methodology: Methods and techniques. Delhi: Dharmesh Art Process.

Mamuya, S. J. (1972). Jando na unyago. East African Publishing House.

Matei, K. A. (2011). Fani ya fasihi simulizi kwa shule za upili. Nairobi: Oxford University Press.

Matinde, R. (2015). Uchanganuzi wa ubabedume katika majigambo (Amabaiko) ya Abakuria (Tasnifu ya Uzamivu, Ndaki ya Laikipia). [Haijachapishwa].

Mbogo, S.N. (2008), Mabadiliko ya maudhui kiwakati katika nyimbo za harusi za jamii ya Waembu, (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta), {Haijachapishwa}

Mlacha, A. K., & Hurskaien, A. (1995). Lugha, utamaduni na fasihi simulizi ya Kiswahili. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI): Dar es Salaam.

Mlambia, M.A. (2017), Kuchunguza dhima za nyimbo za asili za watoto za Wahehe, (Tasnifu ya uzamili, Chuo Huria cha Tanzania), {Haijachapishwa}

Mohamed, F. A. (2016). Kuchunguza mila na desturi za mwanamke wa Visiwani pamoja na fani katika tenzi za Howani na Mwana Kukuwa (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). [Haijachapishwa].

Mussa, J.H. (2023) Dhima ya Nyimbo katika matambikio ya jamii ya watu wa mkoa wa Kusini Unguja, (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania), {Haijachapishwa}

Mutwiri, G. (2005). Mitazamo ya utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigania (M.A. Thesis, Kenyatta University). [Haijachapishwa].

Nandwa, J., & Bukenya, A. (1983). Oral literature for schools. Nairobi: Longman.

Ngure, K. (1998). Aliteracy study of the songs of Joseph Kamaru (B. Ed Thesis, Chuo Kikuu cha Nairobi). [Haijachapishwa].

Rashid, H. U. (2013). Mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao wa Masasi, Tarafa ya Lulindi (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). [Haijachapishwa].

Saleh, K.K. (2015) Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaban Robert: Mfano kutoka Adili na Nuguze na Wasifu wa Siti Binti Saad, (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania), {Haijachapishwa}

Sanken, L. (1976). The oral literature of the Maasai. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Silau, K.G. (2013), Kutathmini dhima ya nyimbo katika kukuza na kuimarisha malezi: Mfano wa kabila la Wakaguru, (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania), {Haijachapishwa}

Simiyu, W. F. (2007). Nyiso za Wabukusu: Mudhui na lugha (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta). [Haijachapishwa].

Sylvester, K. (2015), Mitindo Mamboleo ya ubaadausasa katika nyimboteule za jamii ya Kikalenjini za karne ya ishirini na moja, (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi Eldoret,), {Hijachapishwa}

Wamitila, K. W. (2003a). Fasihi, istilahi na nadharia. Nairobi: English Press.

Wamitila, K. W. (2003b). Kanuni ya fasihi, istilahi na nadharia. Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K. W. (2008). Kichocheo cha fasihi simulizi na andishi. Nairobi: Focus Publications.

Waswa, B, Chai, F, & Buliba, A (2022). Nafasi ya muktadha katika utendaji wa mivigha ya Olubeko miongoni mwa Abanyala wa Kakamega, Kenya. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 5(2), 29–39.

Wathome, R. W. (2009). Mitindo katika nyimbo za tohara za jamii ya Wakamba wa Masaku Tarafa ya Kati (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta). [Haijachapishwa].

Waziri, M. M. (2016). Kuchunguza dhima za nyimbo za Singo katika kijiji cha Uzini Zanzibar (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania). [Haijachapishwa].

Yego, E. K. (2011). Nafasi ya mwanamke: Jinsi inavyotetewa katika nyimbo za Taarab za Zanzibar (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi). [Haijachapishwa].